

**YALIYOMO KWENYE MAKALA**

**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI**





# UTAYARI NA MWITIKIO WA KUKABILIANA NA COVID-19 VIZUIZINI NA MAGEREZANI

## YALIYOMO KWENYE MAKALA



### Utangulizi

Mlipuko wa virusi vya Corona ulitokea mwishoni mwa mwaka 2019 (COVID-19) umeenea kwa kasi ulimwenguni. Tarehe 30 Januari 2020 Shirika la Afya Duniani (World Health Organization - WHO) lilitangaza mlipuko wa Covid-19 kuwa ni hali ya dharura ya afya ya jamii iletayo shaka kimatifa. Tarehe 11 Machi 2020, WHO iliamua kutangaza COVID-19 kuwa janga la kimataifa ikionyesha kusambaa ulimwenguni kwa ugonjwa huu mpya.

Kukabiliana na COVID-19 kunahitaji maandalizi muhimu na utayari wa kuukabili, haswa kwenye vuzuizini au magerezani. Kwa hiyo wafanyakazi wa magerezani wana jukumu muhimu katika kuchangia juhudi za kuzuia kuenea kwa ugonjwa huu na kutengeneza mazingira salama ya magereza na utayari wa kukabiliana na mlipuko huu kwa wakati na kwa njia sahihi.

### Madhumuni ya makala hii

Makala hii imelenga kusaidia maafisa na wafanyakazi wa magereza. Makala hii imeandaliwa kuhakikisha ulinzi na usalama wa wafanyakazi, wafungwa na jamii katika jitihada za kuzuia COVID-19 kuingia magerezani na kupunguza athari utokeapo mlipuko huo. Makala hii inatoa njia za mawasiliano zilizo wazi na kwa taarifa fupi zenye kueleweka.

Katika muktadha huu, kinga ni muhimu sana. Jitihada zote lazima zichukuliwe kuzuia COVID-19 kuingia magerezani. Hatua za kujikinga na kuzuia madhara ya maradhi haya kutapelekea kuvurugika kwa taratibu zilizoeleka za shughuli za magereza. Hii itahitaji uongozi wa magereza kufanya maamuzi magumu yatakayoweza kuathiri operesheni za magereza na shughuli nyingine mbalimbali. Kukabiliana na mlipuko wa COVID-19 pindi kirusi kikishasambaa katika magereza ni changamoto sana haswa kwenye mazingira yenye msongamano mkubwa.

**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI** | **YALIYOMO  
KWENYE  
MAKALA**



Jitihada zote zinapaswa kufanywa kuzuia hali hii sambamba na kuzingatia sera husika kwa mujibu wake na kusimamia haki za binadamu magerezani.

Msongamano mkubwa katika magereza mengi na yenye mazingira machafu yatahishia maradhi haya ya COVID-19 kusambaa kwa haraka na kuwaathiri wafungwa na wafanyakazi wa magereza. Hivyo kipaumbele lazima kitolewe katika kuwapunguza wafungwa. Njia muafaka za utekelezaji wa zoezi hili unapatikana katika mwongozo uliotolewa na idara ya Mahakama na Magereza ya Umoja wa Mataifa.

### **Jinsi ya kutumia makala hii**

Makala hii inajumuisha taarifa kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo WHO, (Preparedness, Prevention and Control of COVID-19 in Prisons and other places of Detention Interim Guidance). Pia US Centres for Disease, Control and Prevention (CDC), (Interim Guidance on Management of Coronavirus Disease 2019 (COVID-19) in Correctional and Detention Facilities).

Taarifa zilizotolewa katika makala hii zinachukua muongozo wa kina ulioanishwa hapo juu na kuweka katika vitendo tayari kutumika. Makala hii siyo kamilifu hivyo yaweza kuhitaji kurekebishwa kulingana na mazingira husika. Kwa taarifa zaidi au muongozo tafadhali rejea vyanzo vilivyotajwa hapo juu au muongozo unaoendana na eneo ulilopo.

Kujiandaa mapema ni muhimu katika usimamizi bora wa haya madhara. Tunashauriwa kutumia taarifa na maelekezo haya mara kwa mara kuwaelimisha maafisa magereza jinsi ya kupambana na maradhi ya COVID-19. Tumia mifano mbalimbali kuyaelezea madhara haya ili kuhakikisha wafanyakazi wote wa magereza wameielewa vema dhana hii ya COVID-19.

**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI**

**YALIYOMO  
KWENYE  
MAKALA**



	<b>Muundo</b>	<b>Yahusu</b>	<b>Wahusika</b>	<b>Matumizi</b>
1	Orodha	Kujiandaa na COVID-19 kwenye magereza	Utawala wa magereza	Magereza
2	Bango	Habari ya jumla ya virusi	Wote	Sehemu mbalimbali zilizopo hapo gerezani
3	Bango	Hatua za msingi za tahadhari	Wote	Sehemu mbalimbali zilizopo hapo gerezani
4	Kadi za mfukoni	Wafanyakazi wa gerezani kwa ufupi	Wafanyakazi wa magereza	Kushirikishana na wafanyakazi wa magereza
5	Bango	Maelezo kwa mfungwa 1&2	Wafanyakazi wa magereza	Shirikisha wafanyakazi wa magereza  Maelezo yaliyotolewa kwa wageni, mabango yaliyowekwa kwenye lango la kuingia gerezani na sehemu zote za wafungwa kukutana na wageni
6	Maelezo / Bango	Maelezo kwa wageni	Wageni	Shirikisha utawala wa gereza
7	Kiandiko cha maelezo	Athari za COVID-19 kwa wafanyakazi wa gereza	Utawala wa gereza	Kushirikishana wakati wa kutoa maelezo kwa wafanyakazi na mabango yaliyopo magerezani
8	Orodha	Utaratibu wa kushughulikia wafungwa	Uongozi na wafanyakazi wa magereza	

**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19**  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI

**KUJIANDAA  
NA COVID-19  
KWENYE MAGEREZA**



### UTAWALA WA MAGEREZA

- Wasiliana Kamishna wa Magereza na kusanya miongozo yote iliyopo kwa ajili ya kudhibiti janga la COVID-19.
- Wasiliana na Waziri wa Afya au Mwakilishi wa Shirika la Afya la Dunia (WHO) nchini na pata taarifa kuhusu :
  - Muongozo kuhusu COVID-19;
  - Mahitaji muhimu kutolea taarifa;
  - Vitu vya kusaidia gereza (vipimio, vifaa vya kinga binafsi (PPE) kwa wafanyakazi, vyumba vya kutengea wafungwa wanaoonyesha dalili za COVID -19)
- Jadili na wachuuzi kuhusu manunuzi makubwa ya chakula, maji, madawa, matibabu, sabuni, vizuia maambukizi na vifaa vingine..
- Andaa taarifa kuhusu idadi ya wafungwa kwenye gereza lako:
  - Tambua wafungwa walio katika hatari kwa kuzingatia au kutozingatia hali zao za kiafya (i.e wazazi waliofungwa pamoja na watoto wao, wafungwa wenye ugonjwa wa kisukari, pumu, feta, wanaougua kifua kikuu (Tb), utapiamlo pia zingatia wazee ambao wapo kwenye hatari ya kuathirika zaidi kama watapata COVID-19;

**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19** | **KUJIANDAA  
NA COVID-19  
KWENYE MAGEREZA**  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI



- Jadili na wizara ya sheria au mamlaka nyingine husika umuhimu wa kupunguza idadi ya wafungwa, vigezo vya kuwapunguza viamuliwe na mahakama au mamlaka husika, kwa kuzingatia wafungwa walio katika hatari, wanaoshikiliwa bila muafaka kamili wa kisheria, wale wanaotumikia vifungo vya muda mfupi, na wenye makosa yasiyohusisha vurugu, wale waliobakiza miezi 6-12 kumaliza vifungo vyao.
- Jadili pia upunguzaji wa wafungwa wapya kwa mamlaka husika za kisheria.
- Kama ni ndani ya mamlaka yako, andaa orodha na zingatia kutolewa mapema zaidi kwa baadhi ya wafungwa au wafungwa walio kwenye makundi maalumu.

Andaa masijala mbili tofauti za dharura:

- Masajili ya kusajili watu wote wanaoingia na kutoka gereza (hii ni pamoja na wafanyakazi wa gereza, wageni wachuuzi na watoa huduma mbalimbali). Taarifa hii itasaidia kwenye tukio la kufuatilia kuenea kwa ugonjwa huu;
- Masajila ya uchunguzi kwa ajili ya kuweka kumbukumbu ya wafungwa wote wanaoonyesha dalili za COVID-19 na kuwatambua wafungwa wote waliokuwa karibu nao angalau mara mbili kwa siku (kufungua na kufunga). Jumuisha vipengele vifuatavyo:
  - Hana dalili inayohisiwa;
  - Ana dalili;
  - Ana maambukizi.

(Mfano wa muundo wa uandishi au usajili umetolewa mwisho wa orodha hii)

**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI** | **KUJIANDAA  
NA COVID-19  
KWENYE MAGEREZA**



- Jadili mipango na mikakati ya kusimamia machafuko na vurugu za wafungwa na usalama wa gereza kama mandamano na majaribio ya kutoroka gerezani. Zingatia kuanzisha mawasiliano na polisi wa kawaida au vyombo vya usalama kwa msaada zaidi..

### **MIUNDO MSINGI NA MATENGENEZO**

- Andaa mchakato na nafasi ya kuchunguza watu wote wanaoingia gerezani kwako. Vituo vya uchunguzi viwe nje kabisa ya lango la kuingia gerezani. Mtu yeyote (mfanyakazi/mgeni/mchuuzi/ au mtoa huduma) anayeonyesha dalili za COVID-19 au ambaye amekuwa karibu na aliyeambukizwa au anayehisiwa kuambukizwa COVID-19, asiruhusiwe kuingia gerezani.
- Anzisha vituo vya kuosha mikono, kwa wafanyakazi, wafungwa na wageni kwenye lango la kuingia gerezani na maeneo yote ya gereza ili kurahisisha unawaji na uoshaji wa mikono na uso wa mara kwa mara.
- Andaa eneo kwa ajili ya kutenga wafungwa wenye dalili za COVID-19. Eneo hilo liwe kwenye jengo tofauti ndani ya gereza (jengo lililojitenga) kama jengo hilo halipo eneo hilo, fikiria mbadala mwingine wa muda kama mahema makubwa yatakayowekwa mbali na maeneo yanayofikiwa mara kwa mara na wafungwa..
- Zingatia kuaanda sehemu ya karantini ya siku 14 kwa wafungwa wapya. Kama hawataonyesha dalili za COVID-19 baada ya siku 14, wahamishiwe kwa wafungwa wengine.



**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19** | **KUJIANDAA  
NA COVID-19  
KWENYE MAGEREZA**  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI



- Anzisha kitengo cha dharura kusimamia wafungwa wanaoonyesha dalili za COVID-19. hii ijumuishe kipengele cha kupata PPE, kumpatia mfungwa barakoa (mask) ya uso na kumpeleka mfungwa eneo lililotengwa. Mfanyakazi wa gereza awe anatambua mchakato huu na aelekezwe na kupewa mafunzo kuhusu mchakato huu.

- Usafi ufanywe mara kwa mara ndani ya gereza:

- Weka dawa ya kuuu viambukizi kwenye maeneo na vitu vinavyoguswa mara kwa mara;
- Weka dawa ya kuuu viambukizi kwenye vitu ambavyo huwa havisafishwi mara kwa mara mfano milango, nondo, vitasa vya milango, swichi za taa, masinki, simu, blanketi na nguo.
- Hakikisha kuna hewa ya kutosha kwa kuondoa viziwi vinavyozuia hewa kupita madirishani, kwenye nondo, milango na uzio na mageti.

## WAFANYAKAZI

- Zungumza/wasiliana na wafanyakazi wa magereza kwamba hatua za kujikinga na kudhibiti COVID-19 vitaathiri kwa muda shughuli za kawaida za gereza.
- Hakikisha wafanyakazi wote wa gereza wana taarifa zote muhimu na wana uelewa wote kuhusu hatua za kujikingana jinsi ya kukabiliana na COVID-19.

**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19**  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI

**KUJIANDAA  
NA COVID-19  
KWENYE MAGEREZA**



- Chunguza wafanyakazi wote kabla hawajaingia gerezani, usiruhusu kuingia iwapo mfanyakazi kaonyesha dalili yeyote ya COVID-19.
- Kama mfanyakazi amekaribiana na mtu mwenye maambukizi ya COVID-19 au mwenye dalili za COVID-19 wape majukumu yatakayowafanya wasikaribiane na wafungwa na wafanyakazi wengine kwa muda wa siku 14 (mfano kufanya doria nje ya gereza au kwenye minara).
- Hamasisha wafanyakazi wawe makini kugundua na kuwasiliana na wafungwa, kuangalia wafungwa wenye dalili za COVID-19 na waweze kutambua tabia yeyote yenye mashaka ya mfungwa itakayosababishwa na vikwazo vilivyowekwa kipindi hiki cha kudhibiti COVID -19.

Punguza shughuli za wafanyakazi wako kwa wafungwa bila vifaa vya usalama:

- Wapange wafanyakazi kwa makundi ya wafungwa wakati wote kuzuia kuenezwa kwa ugonjwa;
- Punguza mawasiliano ya moja kwa moja ya wafanyakazi na wafungwa. Wawasiliane nao kwa mbali (kwa minara , nyuma ya uzio);
- Panga idadi ndogo ya wafanyakazi kufanya kazi kwenye eneo lililotengwa, wapatie PPE muhimu;
- Panga upya majukumu ya wafanyakazi waliopo katika kundi lililo kwenye hatari (vigezo vya kiafya) na punguza mawasiliano yao na wafungwa na wafanyakazi wengine.

**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19**  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI

**KUJIANDAA  
NA COVID-19  
KWENYE MAGEREZA**



Jiandae kwa upungufu wa wafanyakazi:

- Waelekeze wafanyakazi kwa nini ni muhimu kwao kutokuja kazini iwapo wanaonyesha dalili za COVID-19 na weka namna ya kufanya ili waweze kulipwa na wasitozwe faini kwa kutokuwepo kazini;
- Angalia wafanyakazi wachache unaowahitaji kuwepo kwenye gereza lako. Andaa mpango wa kuomba msaada kwa vyombo vingine kusaidia upungufu wa wafanyakazi mfano polisi, jeshi, na wafanyakazi wengine wanaovaa sare;
- Kama itakubalika kwenye mazingira yako, zingatia kutoa mafunzo kwa wafungwa kusaidia kwa muda kuhudumia na kusaidia makundi mengine ya wafungwa.

Jiandae kwa machafuko/vurugu za wafungwa/migomo kutokana na vikwazo vilivyowekwa wakati huu.

Andaa na wafundishe wafanyakazi jinsi ya kutumia vifaa maalumu kwa kujikinga binafsi (PPE).

## WAFUNGWA

Zungumza na wafungwa athari za muda mfupi za COVID-19 kwenye shughuli zao za kawaida (ikiwemo kutembelewa na familia zao na huduma nyingine).

Eleza umuhimu wa kulinda afya ya wafanyakazi, wafungwa na jamii yote kwa ujumla.

**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19** | **KUJIANDAA  
NA COVID-19  
KWENYE MAGEREZA**  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI



- Onyesha wafungwa mabango yenye taarifa na ufafanue taarifa hizo na hakikisha wafungwa wameelewa dhamira ya mabango hayo.
- Wasistize wafungwa kutoa taarifa ya dalili yeyote ya COVID-19 kwa wafanyakazi wa gereza. Hii ni kwa faida ya afya ya kila mmoja.
- Zingatia kupunguza idadi ya wafungwa kukutana kwenye makundi, punguza shughuli za wafungwa na zuia kuchanganya wafungwa kutoka makundi tofauti (haswa wale walio katika kundi hatarishi). Hii inahitaji kupangwa upya.:

- Shughuli za ukarabati/mafunzo ya ufundi/kazi za ufundi;
- Huduma za kidini;
- Harakati au mwenendo wa wafungwa (ndani na nje);
- Kwa shughuli za nje punguza michanganyo ya idara mbalimbali.

### **WAGENI (WACHUUZI NA WATOA HUDUMA)**

- Zungumza na wageni athari za COVID-19 zinavyoweza kusababishwa kwa kutembelea wafungwa mara kwa mara. Hakikisha wanaona na kuelewa taarifa zilizoandikwa kwenye mabango.
- Zingatia kupunguza wageni na fikiria namna nyingine za wafungwa kuwasiliana na wageni , na watoa huduma.

**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19** | **KUJIANDAA  
NA COVID-19  
KWENYE MAGEREZA**  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI



- Anzisha utaratibu wa wageni kutumia simu. Kama italazimu matumizi ya simu, basi weka dawa kwenye vifaa vinavyotumika na vifaa vingine vya umeme mara kwa mara kuua viambukizi.
- Kama wageni wanaleta chakula, mavazi, madawa kwa wafungwa, hakikisha kuna mchakato wa kuhakiki usalama. Kama inawezekana weka dawa ya kuzuia viambukizi na kisha wapatie wafungwa vitu hivyo.
- Kama bado wageni wanaruhusiwa, andaa mchakato wa kuwapima, Usiruhusu mtu yeyote anayeonyesha dalili ya COVID-19 au atakayekataa kufanyiwa uchunguzi kuingia gereza.
- Ongea na wageni na washauri waepuke kugusana na wafungwa kwa faida yao wenyewe na wafungwa na kwa afya za familia zao na jamii kwa ujumla.
- Weka sehemu ya kuosha mikono kwa wageni kwenye lango la kuingia kwenye gereza na lango la kutokea na utoe barakoa (masks) kama ikibidi.
- Hakikisha sehemu ya kukutana na wageni inatoa nafasi ya kutosha (mita mbili kati ya wafungwa na wageni.)
- Tumia masjala ya dharura ya COVID-19 kufuatilia watu wote wanaoingia na kutoka gereza.

**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19** | **KUJIANDAA  
NA COVID-19  
KWENYE MAGEREZA**  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI



## VIFAA

- Orodhesha vifaa vinavyohitajika kudhibiti kuenea kwa COVID-19.
- Ongeza manunuzi ya chakula, maji na madawa.
- Tambua watoaji wa vifaa, fanya manunuzi ya kutosha na hifadhi kwenye ghala kama ikiwezekana.
- Tambua namna ya kuinga sehemu maalumu kama (mapokezi, sehemu za matibabu, jikoni, sehemu za kufulia n.k).
- Zingatia kutumia sekta ya magereza kutengeneza barakoa (masks) na vifaa vingine muhimu. Ikibidi itengeneze viua maambukizi (sanitizer) yenye angalau 60% ya kilevi (kinachoruhusiwa kwa kuzingatia usalama).

**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19** | **KUJIANDAA  
NA COVID-19  
KWENYE MAGEREZA**  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI



**VIFAA VYA KINGA BINAFSI (PPE)**

Vifaa vya kinga binafsi (PPE):



Vizibauso au Barakoa (masks);



Vilinda macho;



Glavu za kutumia kwa muda na kutupa;



Kanzu /gauni za kuvaa kwa muda na kutupa.

Vifaa vingine kwa mahitaji ya kila siku ni kama:



Tishu;



Sabuni za maji au sabuni za miche (hakikisha hazichubui mikono na zinaweza tumika kuosha mikono mara kwa mara);



Vifaa vya kukausha mikono (vya kutumika mara moja na kutupwa) kama karatasi za chooni;



Sanitaiza za mikono zenye angalau 60% ya kilevi, vinavyoruhusiwa kwa kuzingatia usalama;



Vifaa vya usafi, dawa za kuuu viambukizi;



Glavu na mabuti;



Vifaa vya kupulizia dawa za kuuu viambukizi, vinyunyizi, vitavyotumika wakati wafungwa hawapo eneo hilo;



Mifuko ya kuvaa mwilini au mingine (mfuko mkubwa ya mpira).

**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI** | **KUJIANDAA  
NA COVID-19  
KWENYE MAGEREZA**



## **Ushauri kuhusu vizibauso**

Vizibauso au barakoa (masks) za N-95 au FFP-2, vinashauriwa kutumika na wafanyakazi wanaoshughulika moja kwa moja na wafungwa wanaoshukiwa kuwa na COVID-19. Aina hii ya vizibauso ikikaa vizuri kwenye uso inapunguza uwezekanao wa kuvuta maone ya mate au hewa kutoka kwa mgonjwa.

Vizibauso au barakoa za upasuaji zinapaswa kuvaliwa na mtu mwenye COVID-19 au mwenye dalili za ugonjwa huo. Vizibauso hivi vinasaidia kunasa matone ambayo mgonjwa mwenye COVID-19 anaweza kutoa. Kutokana na upungufu wa vizibauso ulimwenguni kote, mbinu mbadala zinatakiwa zichukuliwe japokuwa zinaweza zisiwe na ufanisi unaotarajiwa. Viwanda vidogo vya magereza vinaweza kutumika kutengeneza viziba uso au barakoa mbadala.







# UTAYARI NA MWITIKIO WA KUKABILIANA NA COVID-19 VIZUIZINI NA MAGEREZANI

## HABARI YA JUMLA YA VIRUSI



### NI NINI?

COVID-19 ni janga la kimataifa. Ni ugonjwa uliosababishwa na virusi geni ambayo haikuwa imejulikana kwa binadamu.




### NANI AKO HATIRINI?

Bado tunahitaji kujifunza zaidi juu ya jinsi COVID-19 inavyoathiri watu. Wazee, na watu walio na hali zingine za matibabu, kama vile pumu / ugonjwa sugu wa kupumua, ugonjwa wa sukari na ugonjwa wa moyo au hali yoyote ile ambayo huhatarisha mfumo wa kinga, wanaonekana kuwa katika hatari kubwa.


### DALILI

Mara nyingi, COVID-19 husababisha dalili ikiwa ni pamoja na pua, koo, kikohozi, homa na uchovu wa jumla. Inaweza kuwa kali zaidi kwa watu wengine na inaweza kusababisha nimonia au shida ya kupumua. Katika hali nyingine, maambukizi yanaweza kusababisha kifo.



### HII ITADHURU GEREZA KWA GANI?

Kuzuia COVID-19 kuingia gerezeni itahitaji mabadiliko makubwa ingawaje ya muda mfupi kwa utaratibu wa kawaida wa gereza. Hii inaweza kujumuisha ufikiaji gerezeni, harakati za kuzuia, na shughuli chache za wafungwa. Ingawa inavuruga, hatua hizi za muda ni muhimu kulinda wafanyakazi, wafungwa, na jamii kutoka COVID-19.



### JINSI COVID-19 HUSAMBAZWA?

COVID-19 inaonekana kuenea kwa urahisi kupitia mawasiliano ya karibu na mtu aliyeyambukizwa (umbali wa mita 1). Wakati mtu ambaye ana COVID-19 anapokohoa au kupiga chafya, matone madogo hutolewa na, ikiwa uko karibu sana, unaweza kupumua ndani virusi.



Mtu anaweza kuambukizwa pia kwa kugusa nyuso au vitu vilivyochafuliwa, na kisha kugusa uso wao (kwa mfano mtu anaweza kugusa mhudumu wa afya au kushikana mikono kisha kugusa uso wao wenyewe). Kwa hivyo, kusafisha mazingira kutumia dawa ya kuua viambukizi ni muhimu sana.

**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI**

**HATUA  
ZA MSINGI  
ZA TAHADHARI**




**OSHA**

Osha mikono na sabuni na maji mara nyingi na haswa kabla ya kula na kabla na baada ya kutembelea bafuni.

**ZUIA**

Usiguse uso wako kwa mikono yako. Mikono inagusa nyuso nyingi ambazo zinaweza kuchafuliwa na virusi. Ikiwa utagusa uso wako kwa mikono isiyo safi unaweza kuhamisha virusi kutoka kwa uso hadi kwako mwenyewe.



**ZINGATIA**

Weka umbali wa mwili wa angalau mita 2 kutoka kwa watu wengine (ikiwezekana) na epuka kuguzana yasiyokuwa ya maana ya mwili, haswa ikiwa mtu huyo anakohoa, kupiga chafya au ana homa.

**TAHADHARI**

Ikiwa unakohoa au kupiga chafya, fanya hivyo kwa upinde wa kiwiko chako na sio mkono wako. Njia nyingine ni kufunika kikohozi chako au kupiga chafya na tishu, kisha kutupa tishu kwenye takataka. Katika visa vyote, osha mikono yako kwa sabuni na maji mara moja.



**LINDA**

Ikiwa una dalili zozote za COVID-19 au uone wengine wenye dalili fahamisha msimamizi wa gereza mara moja na utafute matibabu.

**TULIA**

Tulia na ufuate maagizo ya maandishi na ya maneno yaliyotolewa na wafanyikazi wa gereza.



**JINSI YA KUSAFISHA MIKONO?**

 WEKA MAJI MIKONONI	 WEKA SABUNI	 SUGUA MIKONO	 SUGUA NYUMA YA MIKONO	 SUGUA KATIKATI YA VIDOLE	 SUGUA NYUMA YA VIDOLE KWA SEHEMU YA NDANI YA MKONO WA PILI
 OSHA MKONO WA GUMBA	 OSHA MAKUCHA	 SUUZA MIKONO	 PANGUZA NA KITAMBAA	 TUMIA KITAMBAA KUFUNGA BOMBA	 MIKONO YAKO NI SAFI

**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI** | **WAFANYAKAZI  
WA GEREZANI  
KWA UFUPI**



- Zungumza au toa maagizo kwa wafanyakazi na wafungwa kwa kutumia vitendo au amri kwa mbali badala ya kututana moja kwa moja. Fafanua kwa kuonyesha kwa vitendo.
- Kuwa mwangalifu, chunguza na wasiliana na wafungwa kupata taarifa zaidi kuhusu dalili za ugonjwa na kama kuna ishara za vurugu au fujo kati ya wafungwa.
- Andika au toa taarifa ya dalili zote zinazoweza kuwepo kati ya wafungwa na wafanyakazi wengine.
- Epuka kukutana na wafungwa moja kwa moja na kama ikiwezekana fanya utafiti kwa wale wafungwa wasio kwenye kundi hatarishi.
- Tumia lugha ya vitendo, kwa wafungwa hao wasio kuwa kwenye kundi hatarishi.
- Usisimame mbele ya wafungwa kuepuka hatari ya wafungwa kukohoa au kukupumulia moja kwa moja.
- Kama inawezekana, hesabu wafungwa ukiwa kwa mbali.
- Kama italazimka kuwagusa wafungwa, vaa glavu, kinga macho na barakoa au jisafishe kabla na baada kama hakuna glavu.
- Usifanye uchunguzi wa maeneo bila glavu. Kama hakuna glavu jiepuche kabisa kushika sehemu na hakikisha unaosha mikono yako kabla na baada ya uchunguzi huo.
- Hakikisha angalau kuna umbali wa mita mbili kati yako na mfungwa wakati wa kumhoji, kumshauri au wakati wa kuwapokea au kuwaachia wafungwa.

**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI** | **WAFANYAKAZI  
WA GEREZANI  
KWA UFUPI**



- Kama ni ofisini tumia dawati au kiti kutengeneza umbali huo kuwatenganisha.
- Osha vifaa vyako kama radio, simu, pingu, funguo za pingu nk mara kwa mara kwa vizuia maambukizi kama vinapatikana.
- Ikiwezekana badili nguo na viatu kabla ya kwenda nyumbani.
- Kumbusha wafanyakazi kuhusu mazingira magumu ya wafungwa na jukumu lao la kuwahudumia, vile vile operasheni hii iendane na viwango vya haki za binadamu.

**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19** MAELEZO  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI **KWA MFUNGWA 1**



**TULIA**

Afya na usalama wako ni muhimu.

**KUWA MVUMILIVU**

Vizuizi vyovyote, mapungufu, au kufutwa kwa mipango na shughuli za kawaida ni za muda mfupi tu na ni kwa afya na usalama wa kila mtu, pamoja na familia yako na jamii.



**ZINGATIA**

Fuata hatua za tahadhari zilizowekwa kwenye ukuta.

**USAFI**

Ikiwa umemaliza au bweli lako halina vifaa vya usafi waulize wafanyi kazi wa magereza waongeze.



**ULIZA**

Ikiwa wageni wako wanaleta chakula, mavazi na dawa, waulize wafanyakazi wa magereza wafafanua mchakato wa kuacha vitu kama hivyo.




**ULIZA**

Uliza ikiwa kuna njia yoyote ya kuwasiliana na familia yako.



**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19**  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI

**MAELEZO  
KWA MFUNGWA 2**



**TENGENEZA NAFASI**

Ikiwa kuna wafungwa wengi katika seli au bweni lako, tengeneza umbali iwezekanavyo na ulale ukibadilisha nafasi yako ya kulala.

**ZUIA**

Osha mikono, mwili, nguo and matandiko kila mara ukitumia maji na sabuni.



**TAZAMA**

Usifunike dirisha and mlango ya seli. Hakikisha kuna mtiririko wa hewa safi.

**KUWA MWANGALIFU**

Safisha bweni au seli yako mara nyingi Zaidi ukitumia sabuni na maji.




**EPUKA**

Epuka kusirikiana kutumia chupa za maji, vyombo vya kula, sahani na vikombe.



**FUATA**

Tafadhali sikiliza na uheshimu maagizo ya wafanyikazi wa gereza.



**MSAADA**

Ikiwa unajisikia mgonjwa au kuona mfungwa mwingine aliye na dalili, jitenga naye na uripoti kwa wafanyikazi wa magereza mara moja. Ikiwa una maswali yoyote, waulize wafanyikazi wa magereza!

**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19**  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI

**MAELEZO  
KWA WAGENI**




**SHIRIKIANA**

COVID-19 imevuruga ufikiaji wa gereza mara kwa mara. Afya na ustawi wa wafanyikazi, idadi ya wafungwa, na jamii ni kipaumbele.

**FUATA**

Njia ya kawaida ya kutembelea wafungwa inaweza kubadilishwa kwa muda. Tafadhali sikiliza na uheshimu maagizo ya wafanyikazi wa gereza.




**TAHADHARI**

Wageni wote watafanyiwa uchunguzi wa COVID-19; ikiwa unaonyesha dalili ama umekataa kufanyiwa uchunguzi hautaruhusiwa kuingia.

**SIKILIZA**

Tafadhali weka umbali wa mita 2 kutoka kwa watu wengine.



**ULIZA**

Ikiwa unaletea mtu wako vitu za matumizi na ziara zimesimamishwa kwa sababu ya COVID-19, waulize wafanyikazi wakufafanulie jinsi ya kuachia wafungwa vitu.

**ULIZA**

Ikiwa ziara zimesimamishwa, muulize afisa wa magereza ikiwa kuna njia nyingine ya kuwasiliana na mtu wa familia yako.






**UTAYARI NA MCHAKATO MWITIKIO WA KUKABILIANA NA COVID-19**  
**VIZUZIWA NA MAGEREZANI KABLA KUIINGIA GEREZANI**



**1 SEHEMU YA KUNGOJEA**

Jitenge na wengine ukisubiri maagizo.



**2 SEHEMU YA KUWACHA BIDHAA**

Wafanyikazi wa magereza watapokea na kupeleka vitu vyote vinavyoruhusiwa wafungwa.



**3 SEHEMU YA UCHUNGUZI**

Jibu maswali na ukamilishe usajili.



**4 SEHEMU YA USALAMA**

Fuata mazoea ya kulinda usalama.



Wafanyi kazi wa magereza

**A** Iwapo unaweza tembelea mtu wako

**B** Iwapo hauwezi tembelea mtu wako

**C** Iwapo hauwezi tembelea mtu wako

Utaulizwa kuondoka

Utaulizwa kuondoka

Iwapo unaoonyesha dalili

**A** Nenda kazi.

**7 SEHEMU YA KUTOKA**

Kumbuka kuosha mikono yako tena unapotoka gerezeni.



**6 SEHEMU YA KUONA WAFUNGWA**

Zingatia na weka umbali.



**5 SEHEMU YA WAGENI**

Tafadhali nawa mikono ukitumia maji na sabuni.



**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI** | **ATHARI ZA COVID-19  
KWA WAFANYAKAZI  
WA GEREZA**



## UJUMBE

- COVID-19 ni kirusi ambacho tunapaswa kukichukulia umakini mkubwa.
- Utawala wa magereza unafanya kila namna inayowezekana kujaribu kuwalinda wafanyakazi/wafungwa na jamii yote.
- Kama una dalili yoyote ya hivi virusi (homa, mafua, kikohozi, kushindwa kupumua au uchovu) usije kazini ila wasiliana na kamanda wa magereza au kiongozi wako mwingine. Jitenge wewe mwenyewe kwa siku 14 kulinda familia yako, wenzako na jamii ya wafungwa. Piga simu kituo cha afya, kwa muuguzi au kwa daktari kama inawezekana.
- Utaratibu wa kawaida wa shughuli za magereza utabadilika kwa muda (vikwazo vya kutembea hovyovitawekwa, kukutana na wenzako, kuzuiwa kuona wafungwa nk). Inaweza ikapelekea kuchanganyikiwa na msongo wa mawazo kwa wafungwa. Zungumza nao na waelekeze kwamba vikwazo hivyo ni kwa ajili ya kuwalinda wao na familia zao.
- Simamia idadi ya wafungwa, tambua na toa taarifa iwapo kuna hali yeyote ya vurugu au malalamiko ya aina yeyote ya uvunjifu wa amani.
- Ulinzi na usalama ni muhimu kipindi hiki, hata hivyo ili hii ifanikiwe ni vema kuzungumza na wafungwa, kuheshimu utu wao na kuelewa hali yao ya kuchanganyikiwa katika kipindi hiki.

**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI** | **ATHARI ZA COVID-19  
KWA WAFANYAKAZI  
WA GEREZA**



**JINSI YA KUFIKISHA UJUMBE**

- Weka wazi taarifa na hatua zinazochukuliwa haraka iwezekanavyo.
- Usipunguze au kuongeze kiwango cha athari.
- Zingatia sana kuwashirikisha watu wote taarifa muhimu bila kuficha ili kuepuka kufanya watu kuhisi kuna jambo linafichwa.
- Tambua mazingira hatarishi yanayoweza kujitokeza.
- Wafanye wafanyakazi wako wajue unaelewa mahitaji yao na utajaribu kuyafanyia kazi.
- Kuwa mfano wa kuigwa. Kama msimamizi wa gereza, nawe pia unakabiliwa na hatari kama wafungwa na wafanyakazi wengine wa gereza. Chukua nafasi hii kuonyesha tabia ya mfano wa kuigwa:
  - Kuwa mtulivu;
  - Tambua ukali na ugumu wa hatari hii;
  - Kuwa jasiri na mwenye subira;
  - Onyesha tabia ya mfano kwa kufuata ushauri na taratibu zilizoелеkezwa kwa kunawa mikono na kujilinda wewe mwenyewe na wafungwa pia.

**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19** | **UTARATIBU WA  
KUSHUGHULIKIA  
WAFUNGWA**  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI



- Mara tu baada ya mtu kuonyesha dalili za COVID-19, anapaswa kuvaa barakoa (mask) na haraka sana atengwe kwenye sehemu maalumu iliyotengwa haswa kwenye jengo lililotengwa ndani ya gereza hilo.
- Kama huna eneo la kutosha hapo gerezani, wasiliana na vituo vya afya vya karibu au weka mahema yanayoweza kuwekwa uwanjani.
- Ikibidi endelea na zoezi la kutenga watu wote waliokaribiana na wenye maambukizi (kwa kuzingatia mpango wa COVID-19).
- Punguza idadi ya wafanyakazi wanaohudumia wafungwa wenye maambukizi, haswa wale wafanyakazi walio katika kundi hatarishi.
- Mwaga dawa ya kuu viambukizi mara kwa mara kwenye bweni au chumba cha mtu anayehisiwa au aliyehakikishwa kuwa ana maambukizi ya COVID-19.
- Zuia watu kupitapita nje ya eneo lililoteengwa kwa ajili ya walioambukizwa.
- Hakikisha mtu huyo amefunikwa uso wakati wote anapokuwa nje ya kituo hicho kilichotengwa na kila mara anapoingia kiziba uso kibadilishwe angalau kila siku au kinapoonekana kuchafuka au kulowana.
- Wakati wa kutengwa, mtu aliyetengwa awe chini ya uangalizi wa kitabibu angalau mara mbili kwa siku ikiwa ni pamoja na kupima joto lake la mwili na kufuatilia dalili za COVID-19..

**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19** | **UTARATIBU WA  
KUSHUGHULIKIA  
WAFUNGWA**  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI



- Vituo vifanye jitihada zozote zinazowezezana kutenga wote wanaohisiwa kuwa na COVID-19 chini ya uangalizi wa kitabibu wa mtu mmoja mmoja kuwaweka kwenye makundi kufanyike tu kama hakuna namna nyingine inayowezezana.
- Kama kuwaweka makundi ni lazima jaribu kutenganisha waliopimwa na waliohakikishwa kuwa wameambukizwa mbali na wale wanaohisiwa ( wanaonyesha dalili).
- Hakikisha kila mtu anafunika uso na hakikisha wafungwa wote wanaheshimu kukaa mbalimbali mita mbili.
- Wafanyakazi wa gereza wapewe jukumu la kuwafuatilia wafungwa waliotengwa na utawala uhakikishe askari hawa wanapewa kipaumbele kwa matumizi ya PPE.
- Wafungwa waliotengwa ni lazima wapate chakula cha kutosha, mazingira mazuri ya maliwato na mahitaji mengine muhimu.

Dumisha zoezi la kutenga wafungwa wenye dalili na wenye maambukizi hadi vigezo hivi vitakapofikiwa :

- Kwa mtu aliyekwisha pimwa, kuangalia kama bado ana maambukizi:
  - Mtu huyo hana homa kwa masaa 72 bila kutumia dawa za kushusha homa NA
  - Dalili zingine kwa mtu huyo zimekwisha, mfano kukohoa, kushindwa kupumua NA
  - Mtu huyo kupimwa na kukutwa hana maambukizi (negative) kwa kufanyiwa vipimo vya upumuaji angalau ndani ya masaa 24.

**UTAYARI NA  
MWITIKIO WA  
KUKABILIANA NA  
COVID-19** | **UTARATIBU WA  
KUSHUGHULIKIA  
WAFUNGWA**  
VIZUIZINI NA MAGEREZANI



- Kwa mtu ambaye bado hajapimwa ili kuhakiki kama hana maambukizi:
  - Mtu huyo hana homa kwa angalau masaa 72 bila kutumia dawa za kushusha homa NA
  - Dalili zingine kwa mtu huyo zimekwisha mfano; kukohoa, ugumu kwenye kupumua NA
  - Angalau siku saba zimepita tangu dalili ya kwanza kuonekana.
  
- Kama mfungwa mwenye COVID-19 anaachiwia kutoka kifungoni wakati bado yupo kwenye kipindi cha kutengwa wasiliana na vituo vya Afya vya Umma kuangalia namna ya kumsafirisha na kumuendeleza na matibabu muhimu na kuendelea kumtenga.
  
- Kama kuna kifo gerezani:
  - Maiti hiyo ni wazi yaweza kuwa na wadudu wa COVID-19 kwa siku nyingi;
  - Funga maiti kwenye mfuko maalum au mbadala mwingine kama mfuko mkubwa wa plastiki;
  - Hifadhi kwenye chumba chenye ubaridi kama mochwari ya muda;
  - Kama hakuna namna nyingine choma maiti hiyo ndani ya saa 12 ila kwa kuzingatia sana taratibu za kidini za marehemu au familia zao;
  - Weka kumbukumbu ya picha kama inawezekana na toa taarifa ya kifo kwa mamlaka husika na fuata taratibu zilizowekwa za vifo kwenye gereza.



**YALIYOMO KWENYE MAKALA**  
**UTAYARI NA**  
**MWITIKIO WA**  
**KUKABILIANA NA**  
**COVID-19**  
**VIZUIZINI NA MAGEREZANI**

Justice and Corrections Service  
Office of Rule of Law and Security Institutions  
United Nations Department of Peace Operations  
[dpo-jcs@un.org](mailto:dpo-jcs@un.org)

Division for Peace  
United Nations Institute for Training and Research  
[ptp@unitar.org](mailto:ptp@unitar.org)

**#KnowledgeToLead**

